# UMOJA - JARIDA

UNITED NATIONS
TANZANIA

Toleo la 90
Mei - Juni 2020


## WHO YATOA VIFAA TIBA NA DAWA ILI KUKABILI JANGA LA COVID-19 ZANZIBAR




Ofisa wa Mawasiliano na Ushirikiano wa WHO, Dkt. Ghirmay Andemichael, akikabidhi dawa na vifaa tiba kwa Mkurugenzi Mkuu wa Huduma za Afya ambaye pia ni mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Taifa cha Kukabiliana na COVID-19 cha Wizara ya Afya, Zanzibar, Dkt. Jamala Taib.
***Picha | Agnes Kenneth/ UN Tanzania***

## VIDOKEZO

- WHO Tanzania yatoa msaada wa kiufundi kwa Zanzibar kwa ugatuzi wa juhudi za kukabiliana na COVID-19
- WFP, Japan zashirikiana kukabiliana na utapiamlo nchini Tanzania
- COVID-19 yaibua ubunifu katika kukomesha ajira mbaya kwa watoto Tanzania
- Kila mmoja anaweza kuleta tofauti, mchango wa kila mmoja una maana kubwa

Hadi kufika tarehe 29 Juni, 2020, janga la COVID-19 lilikwishautikisa ulimwengu kwa kusababisha jumla ya watu walioambukizwa kufikia 10,021,401 na takribani watu nusu milioni (499,913) wakifariki dunia. Idadi ya wagonjwa na vifo kote duniani na hata katika Ukanda wa Afrika inazidi kuongezeka. Kama sehemu ya kuimarisha Kanuni za Afya za Kimataifa (IHR) Uwezo wa Msingi na kuimarisha mfumo wa huduma muhimu za matunzo, Shirika la Afya Duniani (WHO) nchini Tanzania limetoa wataalamu wa kiufundi, vifaa tiba, dawa na seti kamili za uwezeshi ili kuanzisisha Kituo cha Uendeshaji Huduma za Dharura za Afya ya Jamii (Public Health Emergency Operations Center (PHEOC)) upande wa Zanzibar.

Kama mwendelezo wa uimarishaji mfumo wa huduma muhimu za matunzo, kuimarishwa kwa Huduma za Kinga na Udhibiti dhidi ya Maambukizo na kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji ili kupambana na COVID-19 upande wa Zanzibar, WHO ililipia manunuzi ya vifaa tiba 36, dawa na vifaa vya ufuatiliaji vilivyokabidhiwa kwa Wizara ya Afya, Zanzibar. Vifaa hivyo ni pamoja na vitanda vya wagonjwa, vifaa vya kitabibu vya kujikinga na maambukizo, na vifaa vya kuhudumia wagonjwa, miongoni mwa vitu mbalimbali. Gharama jumla ya hisani hiyo ni Shilingi za Tanzania 95,657,500.00 sawa na Dola za Marekani 41,992.00.

*Inaendelea Ukurasa wa 2*

*Kutoka ukurasa wa 1*

Katika sherehe hizo za makabidhiano, Ofisa Mratibu Mawasiliano wa WHO, Dkt. Ghirmay Andemichael aliishukuru Wizara ya Afya na Serikali ya Zanzibar kwa usimamizi na ushirikiano wa karibu na WHO na Mfumo wa UN kwa ujumla na alirudia kueleza kwamba ushirikiano na msaada wa kujenga uwezo wa kuzuia, kushughulikia na kudhibiti dharura za kiafya utaendelea. Alikumbushia kwamba vifaa tiba vinakusudiwa kuimarisha uwezo wa Zanzibar kuendana na kitisho cha janga la COVID-19, kuimarisha matunzo muhimu ya afya na kuwapa kinga wafanyakazi katika sekta ya afya wasipatwe na maambukizo. Alisisitiza kwamba hatupaswi kuonyesha ulegevu, kwani janga hilo halionyeshi dalili za kupungua na alishauri kwamba ni muhimu kila mtu awajibike katika kuzingatia maelekezo ya serikali na hatua zinazopendekezwa ili kuzuia kuenea kwa virusi. Ni ushirikiano wetu wa pamoja utakaosaidia kulishinda janga hili. Aliongeza kwamba tabia chanya tunazozitumia wakati wa janga hili ndizo zitakazokuwa na matokeo chanya ya kuzuia magonjwa mengine ya kuambukiza kama vile kipindupindu.

Mchango huo wa vifaa mbalimbali ulipokelewa na Mkurugenzi Mkuu wa Huduma za Afya na mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Taifa cha Kukabili COVID-19 cha Wizara ya Afya, Zanzibar, Dkt. Jamala Taib. Mkurugenzi Mkuu aliishukuru WHO na Mfumo wa UN nchini kwa ushirikiano wa muda mrefu huku akisisitiza kwamba vifaa tiba na dawa vilivyonunuliwa kupitia UN nchini Tanzania vitakuwa na msaada mkubwa sana katika kuimarisha juhudi za Serikali za kuimarisha hufuma za afya na kukabili janga hili kwa ufanisi mkubwa.

## JANGA LAATHIRI JUHUDI ZA KUKOMESHA TOHARA KWA WANAWAKE



Wasichana wa umri wa balehe wakitembelea kituo rafiki kwa vijana kabla ya kuibuka kwa janga la COVID-19 nchini Tanzania. ***Picha| Karlien Truyens/UNFPA Tanzania***

Kwa msaada wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), asasi isiyo ya kiserikali ya 'Matumani kwa Wasichana na Wanawake' ya nchini Tanzania inaendesha nyumba salama mbili katika wilaya za Serengeti na Butiama mkoani Mara kwa ajili ya wasichana waliokimbia kufanyiwa tohara makwao. Pamoja na kwamba utamaduni huo umeharamishwa nchini Tanzania tangu mwaka 1998 na ahadi ya serikali ya kutimiza na kufikia lengo la dunia la kukomesha kabisa vitendo vya ukatili kwa msingi wa

*Inaendelea Ukurasa wa 3*

*Kutoka ukurasa wa 2*

kijinsia (GBV) vitendo kama vile vya tohara, kama inavyoshuhudiwa na Mpango wa Taifa wa Kuchukua Hatua Kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto, asilimia 32 ya wanawake na wasichana (wenye miaka kati ya 15 na 49) katika mkoa huo wamefanyiwa tohara.

Mwezi Machi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitangaza kufungwa kwa shule kuanzia zile za chekechea hadi sekondari kwa muda wa siku 30 ili kukabiliana na kuenea kwa janga la COVID-19; hii ilikuwa baada ya vyuo vyote vikuu, vya kati na vile vya ufundi kuwa vimefungwa kwa sababu hiyohiyo.

Kama ilivyo kwa nchi nyingine katika ukanda huu, janga la COVID-19, na hatua zilizofuatia za kuzuia shughuli za kibinadamu, lina uwezekano mkubwa wa kuathiri vibaya juhudi za kumaliza tohara ya wanawake nchini Tanzania, jambo ambalo Rhobi Samwelly, mwanzilishi wa Shirika la Matumaini kwa Wasichana na Wanawake, tayari analishuhudia.

Msimu wa tohara katika mwaka kwa shughuli zilizo nyingi kuhusiana na tohara ya wanawake hufanyika mkoani Mara mwezi Desemba, lakini tayari shirika hili limekwishawaokoa wasichana 62 waliokuwa katika hatari ya kufanyiwa vitendo hivyo. Walishindwa kuwafikia wasichana wengine 60 ambao tayari walikwishafanyiwa tohara. Maelezo kutoka kwa Valerian Mgani, anayetoka katika asasi ya Association for the Termination of FGM, ambalo pia liko mkoani Mara, naye anatoa simulizi kama hiyo ambapo hadi kufikia Machi, wasichana 27 walikwishafanyiwa tohara, jambo ambalo Valerian anasema hakuwahi kulishuhudia huko nyuma.

Janga hili pia linaleta athari nyingine, ambayo haisikiki sana kwenye vyombo vya habari, lakini inaweza kuathiri vibaya sana juhudi za kukomeasha tohara ya wanawake: rasilimali ambazo tayari hazitoshelezi na sasa zinakuwa na matumizi mengi zaidi. Asasi ya Hope for Girls and Women zinawapa wasichana zinaowaokoa mafunzo ya ufundi na pia kuwasaidia wasichana kwa kuwalipia ada na gharama nyingine za kukaa bwenini katika shule wanakosoma. Lakini kufuatia kufungwa kwa taasisi za elimu, wasichana walilazimika kurudi kwenye makazi salama, jambo linalomaanisha kwamba kuna watu wengi zaidi wa kulisha na wasichana wengi zaidi wa kuwapa hifadhi.

Nyumba salama za Butiama na Serengeti kwa pamoja zina uwezo wa kuhifadhi watu 100, lakini hivi sasa zina wasichana 187. Nyumba salama ya ATFGM Masgana nayo pia ina jumla ya wasichana 187 ingawa idadi imepungua kiasi tangu kufunguliwa kwa vyuo vikuu, vyuo vya kati na vile vya ufundi pamoja na wanafunzi wa Kidato cha 6 tangu tarehe 1 Juni.

Mwaka 2020 ni wa kwanza katika Mkakati wa Kuchukua Hatua wa Muongo (the Decade of Action), ambapo imebaki miaka 10 tu ya kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Ajenda ya Mwaka 2030 ikiwemo kukomesha kabisa vitendo vya ukatili wa kijinsia na tabia nyingine za kikatili kwa kila mmoja, kila pahali. Kadiri tunavyoendelea, UNFPA na washirika wake wataongeza na kukuza zaidi juhudi kuhakikisha mafanikio yaliyokwishapatikana katika kufikia malengo ya kitaifa na dunia katika kukomesha tohara ya wanawake nchini Tanzania hayakwami au mbaya zaidi kurudi nyuma, na badala yake inaweka mkazo katika kuimarisha zaidi.

# WFP, JAPAN ZASHIRIKIANA KUKABILIANA NA UTAPIAMLO NCHINI TANZANIA



Benki ya Jamii za Vijijini (VICOBA) katika Kijiji cha Nduu inayosaidiwa na Programu ya Boresha Lishe. ***Picha* | *WFP/ Mwanzo Millinga***

Serikali ya Japani imetoa mchango wa Dola za Marekani milioni 1.5 kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) ili kusaidia uekelezji wa mradi wa miaka minne (2017-2021) wa Boresha Lishe katika vijiji kwenye Kanda ya Kati nchini Tanzania.

Mradi wa Boresha Lishe unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na Japan unalenga kuimarisha upatikanaji na matumizi ya chakula chenye virutubisho kwa wanawake na watoto wapatao 30,000 kupitia mawasiliano ya mabadiliko ya tabia za kijamii, utoaji wa vyakula vyenye virutubisho maalumu katika wilaya za Bahi na Dodoma mkoani Dodoma na wilaya za Ikungi na Singida Vijijini mkoani Singida.

Mradi huo unalenga kuimarisha maarifa kuhusu lishe, mtawanyiko wa vyakula bora na maji, usafi wa mazingira na tabia za usafi binafsi (WASH). Vilevile, kuna juhudi za kuhamasisha ufugaji wa ngazi ya kawaida, kilimo cha mseto na uendeshaji wa Vikundi vya Benki za Jamii (VICOBA), kukuza upatikanaji wa mtaji na vilevile vyakula vyenye lishe.

Kwa mchango wa Serikali ya Japan, WFP inatoa na kufunga vituo vidogovidogo vya nishati ya jua kwa ajili ya VICOBA 40 zilizo chini ya mradi huu. Vituo hivyo vina vifaa vya kukodisha vinavyoweza kuongezewa tena na tena umeme kama vile kandiri na vituo vinaendeshwa kibiasahra ili kutoa fursa ya kipato kwa VICOBA na wanachama wa vikundi hivyo.

Ili kusambaza na kufunga vituo hivyo vya umeme wa sola, WFP inashirikiana na kampuni binafsi ya Japan, ikitumia ujunzi wake uliopatikana katika uendeshaji wa biashara za namna hiyo kwa miaka mingi.

# COVID-19 YAIBUA UBUNIFU KATIKA KUKOMESHA AJIRA MBAYA KWA WATOTO TANZANIA



Mkutano wa majadiliano unaohusisha ILO, AZAKI na wanajamii wakiwa Ndevelwe, Tabora. ***Picha | ILO Tanzania***

Dunia imepiga hatua kubwa katika kumaliza ajira mbaya za watoto. Katika miongo miwili iliyopita, takribani watoto milioni 94 wameondolewa kwenye ajira ngumu. Furaha ya juhudi hizi kubwa zilipunguzwa kasi na janga la COVID-19. Kuna changamoto mpya zinazojitokeza hususan kufuatia kupunguzwa na kufungwa kwa shughuli za kiuchumi na kijamii (lockdowns) jambo linalotishia kuongezeka tena kwa ajira mbaya za watoto, unyanyasaji wa watoto na wanafunzi kukatisha masomo yao pale shule zitakapofunguliwa. Ujumbe wa dunia kwa Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ajira Mbaya za Watoto kwa Mwaka 2020 (WDACL), inayoadhimishwa kila tarehe 12 Juni, ulikuwa: "COVID-19: Ongeza bidii ya kuwalinda watoto dhidi ya ajira za watoto hivi sasa zaidi kuliko zamani!" Utekelezaji wa ujumbe huu uko bayana mkoani Tabora ambako COVID-19 inatia moto juhudi za kukabiliana na tatizo la ajira za watoto.

Juhudi za kumaliza ajira mbaya za watoto mkoani Tabora zinapigiwa chapuo na Mkuu wa Mkoa, Mh. Aggrey DJ Mwanri, ambaye pia ni mlezi wa shughuli za ulinzi wa watoto mkoani humo. Kwa msaada wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), ofisi yake kupitia mradi unaoendelea wa 'Kukabili Upungufu wa Kazi zenye Hadhi katika Sekta ya Tumbaku' (Addressing Decent Work Deficits in the Tobacco sector (DWiT)) sambamba na wadau wengine wa ajira ya watoto wametoa fedha ili kuendesha vipindi vya mafunzo kwa njia ya redio kwa jina la Tabora Darasa Plus. Vipindi hivi hutolewa katika mazingira yanayofanana na ya darasani kwa ajili ya wanafunzi walio nyumbani kwa sababu ya COVID-19 na hivyo kuwafikishia watoto wa kuanzia chekechea hadi kidato cha nne wiki nzima. Vipindi hivyo hurushwa kupitia redio za jamii na huwafikia takribani karibu asilimia 50-60% ya wanafunzi mkoani humo katika kipindi ambapo shule zimefungwa na hivyo kuwasaidia watoto kuendelea kujifunza wakati wa janga.

*Inaendelea Ukurasa wa 6*

*Kutoka ukurasa wa 5*

Kati ya Machi na Juni, 2020, sheria ndogondogo katika ngazi ya kata zimepitiwa upya ili kushughulikia tatizo la ajira ya watoto. Mapitio hayo yamejumuishwa katika kampeni za ngazi ya jamii ya uhamasishaji zilizoendeshwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) kupitia mradi wa DWiT wa ILO kuhusu umuhimu wa kuwalinda watoto hasa katika kipindi hiki cha janga.

Maadhimisho ya WDACL yamekuja katika wakati sahihi ili kuimarisha juhudi zinazoendelea. Miongoni mwa mambo mengine, ILO kwa kushiriniana na wadau na washirika, kama vile Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, TUCTA na ATE limewakumbusha wadau na jamii kuweka mkazo na kuhakikisha kwamba Lengo la 8 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (Kazi zenye Hadhi na Ukuaji wa Kiuchumi), hasa shabaha ya 8.7 ya kuondoa aina zote za ajira mbaya kwa watoto hapo ifikapo mwaka 2025, linafikiwa.

## KILA MMOJA ANAWEZA KULETA TOFAUTI, MCHANGO WA KILA MMOJA UNA MAANA KUBWA




Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Bw. Zlatan Milisic, akiwahutubia wageni walioshiriki katika majadiliano mubashara ya Siku ya Wakimbizi Duniani yaliyoendeshwa na paneli maalumu jijini Dar es Salaam. ***Picha | UNHCR Tanzania***

Katika mwaka 2020, Siku ya Wakimbizi Duniani (WRD) iliadhimishwa huku kukiwa na mabadiliko makubwa mno ya kijamii. Siyo tu kwamba watu wengi zaidi walikuwa wakikabiliwa na hali ngumu baada ya kukimbia makwao kwa ajili ya kutafuta usalama bali dunia nzima ilikuwa ikididimia kwenye hatari kubwa kwa sababu ya janga la COVID-19.

Nchini Tanzania, kama ilivyokuwa katika nchi nyingi, maadhimisho yale yaliyozoeleka ya pamoja ambayo yangewakutanisha watu wengi pamoja hayakuwezekana kwa sababu ya COVID-19. Hata hivyo, kupitia mfululizo wa shughuli mbalimbali na uendeshaji wa maadhimisho kwa njia za mtandao, Umoja wa Mataifa, pamoja na

*Inaendelea Ukurasa wa 7*

*Kutoka ukurasa wa 6*

Serikali na washirika wengine, walifanikiwa kuikumbusha dunia kwamba kila mmoja, wakiwemo wakimbizi, wana mchango wanaoweza kuutoa kwa jamii.

Njia hiyo ya kiubunifu ya kuadhimisha tukio hilo, ambayo ilihusisha kuchanganya shughuli mbalimbali kupitia satelaiti na kampeni za mitandao ya kijamii kwa kuwatumia waandishi maarufu na watu maarufu wa hapa nchini, kulisaidia kujenga mazingira kwa ajili ya tukio kubwa, ambalo lilitangazwa mubashara kwa mamilioni ya Watanzania na hadhira ya kimataifa. Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mtaifa, Bw. Zlatan Milišić, alitoa hotuba ya ufunguzi ambayo ilifuatiwa na mijadala kupitia kikundi cha majadiliano. Wanavikundi walikuwa ni pamoja na wawakilishi wa Serikali, Shirika la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), wasomi, vyama vya kiraia, asasi zisizo za serikail na mkimbizi.

Bw. Milišić alitambua na kushukuru ukarimu wa jamii na nchi mbalimbali zinazowahifadhi wakimbizi. “Kwa niaba ya familia ya Umoja wa Mataifa, ninaishukuru Serikali na Watu wa Tanzania kwa ukarimu wao. Hasa, jamii za watu wa Kigoma ambao wamekuwa wakiwahifadhi wakimbizi kwa miongo mingi na hivyo kujikuta nao wakikabiliwa na changamoto zao nyingi za kijamii na kiuchumi.”

Tanzania imekuwa nchi ya kupigiwa mgano katika masuala ya amani na utengemao katika ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika na ina utamaduni wa muda mrefu wa kuwapokea na kuwapa wakimbizi hifadhi. Hivi sasa, nchi inawapa hifadhi zaidi ya wakimbizi 283,000, wengi wakiwa ni kutoka Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Mwakilishi wa UNHCR nchini Tanzania, Bw. Antonio Canhandula, alitoa wito kwa umma kutafakari madhira wanayopata wakimbizi. Alieleza kwamba katika kipindi hiki cha janga la COVID-19, wakimbizi walikuwa katika hatari kubwa zaidi lakini alipongeza ujasiri wao na utayari wao wa kujiunga katika juhudi za kupambana na virusi vya corona.




Kiongozi wa wakimbizi katika Kambi ya Nyarugusu, Bi. Angelique Abiola, akiongoza mjadala kati ya wakimbizi na mashirika ya misaada ya kibinadamu kuhusu masuala yanayowaathiri wakimbizi. Hii ilikuwa katika maadhimisho ya Siku ya Wakimbizi Duniani. ***Picha | UNHCR Tanzania***

***Inaendelea Ukurasa wa 8***

*Kutoka ukurasa wa 7*

"Ningependa kuwaalika nyote kutumia muda kidogo kutafakari na kutambua hata vile vitendo visivyoonekana sana vya ujasiri wa wakimbizi ambao wako katika mstari wa mbele kupambana na janga hili sambamba na wenyeji wao pamoja na wafanyakazi watoa misaada. Wapo ambao wanatumia ujuzi wao wa kushona ili kutengeneza barakoa kwa ajili ya wenzao. Wengine wanafanya wajibu muhimu katika kutoa taarifa kwa umma pamoja na elimu," alisema.

Katika mkoa wa Kigoma, unaohifadhi wakimbizi, matukio mengine kwa njia ya satelaiti yalifanyika. Katika Kambi ya Wakimbizi ya Nduta, UNHCR na Washirika waliandaa maonyesho ya kujipatia riziki katika Ofisi za Shirika la HelpAge. Katika Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu, vipindi 26 vya majadiliano vilifanyika. Mada ziligusa masuala yanayowaathiri wakimbizi, kama vile umuhimu wa uzazi wa mpango, jinsi jamii zinavyoweza kukabili malaria, elimu, na mazingira. Vilevile, watoto kutoka katika Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu na jamii za wenyeji walishiriki katika mashindano ya Sanaa yaliyofuatiwa na mijadala iliyoongozwa na wanapaneli. Mijadala hiyo ilihusu masuala ya wakimbizi.

Siku hii ni siku ya kimataifa iliyoanzishwa na Umoja wa Mataifa ili kuenzi wakimbizi kote duniani. Kila mwaka siku hii inaadhimishwa tarehe 20 Juni na hushangilia uimara na ujasiri wa watu ambao wamelazimika kukimbia makwao kwenda katika nchi nyingine ili kuepuka migogoro au mateso.

Ukiachia mbali maadhimisho ya siku hii, Umoja wa Mataifa na washirika wanaendelea kuomba kila mmoja kutoa msaada ili kuendeleza juhudi za dunia za mshikamano na utekelezaji. Kila mmoja anaweza kuleta tofauti, na mchango wa kila mmoja una maana katika juhudi za kujenga dunia iliyo na haki zaidi, iliyo jumuishi zaidi na yenye usawa.




Maonyesho ya njia za kujipatia riziki yaliyofanywa na wanawake kupitia mradi wa Kikapu Ili Kuleta Ufumbuzi (Basket for Solution) katika maadhimisho ya mwaka huu ya Siku ya Wakimbizi Duniani (#WorldRefugeeDay) yaliyofanyika katika Kambi ya Wakimbizi ya Nduta. ***Picha | UNHCR Tanzania***

***Inaendelea Ukurasa wa 9***

*Kutoka ukurasa wa 8*

*"Kwa niaba ya familia ya Umoja wa Mataifa, ninaishukuru Serikali na Watu wa Tanzania kwa ukarimu wao. Hasa, jamii za watu wa Kigoma ambao wamekuwa wakiwahifadhi wakimbizi kwa miongo mingi na hivyo kujikuta nao wakikabiliwa na changamoto zao nyingi za kijamii na kiuchumi."*

**Bw. Zlatan Milišić, Mratibu Mkuu wa Shughuli za Umoja wa Mataifa Tanzania**



Washiriki wa majadiliano katika Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu. ***Picha | UNHCR Tanzania***

## WANAGENZI WA ILO WAANZA TENA MAFUNZO YALIYOSIMAMISHWA NA COVID-19

*Taasisi za mafunzo nchini Tanzania Bara na Zanzibar zimeanzisha upya Programu ya Uanagenzi katika Tasnia ya Hoteli baada ya kusimamishwa kwa muda kutokana na COVID-19.*

Zaidi ya vijana 200 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar wameanza upya kushiriki katika Pogramu ya Uanagenzi katika Tasnia ya Hoteli baada ya kusimamishwa kwa miezi miwili kutokana na janga la COVID-19.

Kampasi za Chuo cha Taifa cha Utalii (The National College of Tourism (NCT)) upande wa Bara zilifunguliwa mnamo Juni 1, 2020 wakati State University of Zanzibar Institute of Tourism (SUZA IoT) kilifunguliwa Juni 22 kufuatia kusimamishwa kwa masomo katika taasisi zote za elimu mnamo Aprili 15, 2020.

Taasisi za mafunzo ni mdau muhimu wa ILO katika Programu ya Uanagenzi, ambayo lengo lake kubwa ni kutoa mafunzo kazini na fursa za ajira katika sekta ya hoteli nchini Tanzaina, hasa kwa vijana wa Tanzania wasio na tegemeo lingine. Zaidi ya asilimia 70 ya wanufaika wa programu hii walipata ajira za kudumu katika baadhi ya hoteli kubwa nchini ndani ya muda wa miezi mitatu tangu walipohitimu mafunzo. Programu inawapa wanagenzi mafunzo ya miaka miwili ambapo miezi sita hutumika katika taasisi za mafunzo na miezi 18 huwa mafunzo kwa vitendo katika mahoteli.

Kwa kuwa janga la COVID-19 limevuruga programu ya mafunzo kipindi hiki, ILO pamoja na washirika NCT na SUZA IoT, imebuni masuluhisho ili kuwapa wanagenzi mafunzo ya kiukamilifu kama programu inavyokusudiwa kufanya. "Hatuna uhakika ni lini hasa wanagenzi watarejea katika maeneo yao ya mafunzo kwa vitendo kwani hoteli nyingi na nyumba za wageni bado hazijaongeza kasi katika uendeshaji wa biashara zao. Kwa hiyo, ni kazi yetu kuhakikisha kwamba wanagenzi wanaorejea wanapata mafunzo ya nadharia na ya vitendo kwa ukaribu kadiri inavyowezekana," anasema Mkurugenzi wa SUZA IoT, Dkt. Aley Nassor. Pamoja na msaada kutoka ILO,

*Inaendelea Ukurasa wa 10*

*Kutoka ukurasa wa 9*

wanataalamu vinara katika tasnia hii kama vile wapishi, mameneja wa huduma za vyumbani na wakufunzi watatoa mafunzo ya kina kwa vitendo kwa wanagenzi katika vyuo.

ILO inapanga kuendelea na mpango wake wa msaada katika kukabili COVID-19 mara pale mahoteli yatakapokuwa tayari kuwapokea wanagenzi. "ILO itazipa motisha hoteli washirika ili ziendelee kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanagenzi kwa kubeba gharama za posho za wanagenzi hasa kwa sababu ya vurugu iliyosababishwa na janga katika sekta ya utalii na mahoteli," anasema Ofilsa wa ILO anayeshughulika na Programu ya Taifa ya Ujuzi, Comoro Mwenda.

Huku bado COVID-19 ikiwa ni tishio duniani, sekta nyingi, hasa utalii na mahoteli ziko katika hatari. Programu ya Ujuzi ya ILO inafanya kazi kujaribu kupunguza makali ya madhara ya muda mfupi na mrefu ya janga kwa programu ya uanagenzi katika biashara ya utalii na mahoteli. "Njia ya kiubunifu ni muhimu ili kusaidia kukabili changamoto zinazoletwa na COVID-19 katika programu hii," alisema Bw. Mwenda.

Programu ya Uanagenzi inafadhiliwa na Serikali ya Norway, na ni sehemu ya Tawi la ILO la Ujuzi na Kuajirika, ambalo linalenga kutoa msaada wa kiufundi kwa washirika wa kijamii wa Tanzania katika kuhamasisha mafunzo yanayotoa ujuzi na kusaidia upatikanaji wa ajira katika soko la ajira.



Mafunzo kwa wanagenzi yenye mkazo katika namna ya kuishi baada ya kurejea kutoka kwenye mapumziko yaliyosababishwa na COVID-19 na mbinu za kujikinga. ***Picha | ILO Tanzania***



Wanagenzi warejea katika vyuo vyao ili kupata mafunzo kwa vitendo ambayo huandaliwa kupitia programu ya wanagenzi tayari kwa mafunzo kwa vitendo zaidi katika hoteli washirika. ***Picha | ILO Tanzania***

*"ILO itazipa motisha hoteli washirika ili ziendelee kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanagenzi kwa kubeba gharama za posho za wanagenzi hasa kwa sababu ya vurugu iliyosababishwa na janga katika sekta ya utalii na mahoteli,"*

**Comoro Mwenda, Ofisa wa ILO anayeshughulika na Programu ya Taifa ya Ujuzi**

# WFP, UBELGIJI ZAWAUNGANISHA WAKULIMA WA TANZANIA NA SOKO LA CHAKULA LA WAKIMBIZI



Kwa mwendo wa saa kutoka juu kushoto: maharage aina ya 'Rose coco', 'red kidney', na maharage ya njano WFP hununua aina mbili za kwanza. Hayo yanalimwa kibiashara chini ya Mradi wa Enabel. ***Picha | WFP/Max Wohlgemuth***

Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula (WFP) na Enabel, ambalo ni Shirika la Maendeleo la Ubelgiji, yameungana ili kufungua milango kwa soko jipya kwa wakulima kutoka mkoani Kigoma na kuwasaidia majirani zao walio wakimbizi.

Shirika la Enabel linashirikiana na wakulima 15,000 kutoka Mkoa wa Kigoma chini ya Mradi wa Kilimo Endelevu Mkoani Kigoma. Kwa kutumia nia ya uendelezaji mnyororo wa thamani unaolenga kuwasaidia 'maskini', wakulima wanajikuta wakisaidiwa katika mnyororo mzima kuanzia uzalishaji hadi uhifadhi na utafutaji masoko. Upatikanaji wa fedha unawasaidia wakulima kununua vitu kama vile mbegu bora, viutatilifu na mbolea huku wakipata mafunzo kuhusu mbinu bora za kilimo ili kuongeza wingi na ubora wa mazao yao.

Takribani kilometa 15 kutoka katika mashamba yanayosaidiwa na Enabel, kuna Kambi ya Wakimbizi ya Mtendeli – ambayo ni kimbilio la kihistoria la wakimbizi na wanaotafuta hifadhi wanaotoka nchi jirani. Kambi hiyo ilifunguliwa upya mwaka 2016, kufuatia ongezeko la wakimbizi kutoka Burundi na hivi sasa ina zaidi ya wakimbizi 30,000. Nchini Tanzania, wakimbizi wanazuiwa na sera kali inayowataka kukaa kambini tu huku kukiwa na fursa kidogo za kujikimu na fursa za kujipatia riziki. Kwa hiyo wanategemea zaidi jamii ya kibinadamu kuwapatia mahitaji yao ya msingi kama vile chakula. WFP huwapa wakimbizi nafaka, jamii ya kunde (yakiwemo maharage), mafuta ya mbogamboga, vyakula vyenye lishe maalumu na chumvi ili kukidhi kiwango cha chini ya mahitaji yao ya chakula kwa siku.

"WFP ni mnunuzi mkubwa wa bidhaa za chakula kinachozalishwa nchini Tanzania," anasema Bw. Michael Dunford, Mwakilishi wa WFP nchini Tanzania. "Kwa kushirikiana na Enabel, WFP sasa itasaidia kufungua milango kwa soko jipya kwa wakulima wadogo katika jamii za wenyeji ambao watanufaika na msaada wa WFP kwa wakimbizi. Kwa mafanikio ya manunuzi haya, WFP itaendelea kupanua kupitia manunuzi zaidi ya moja kwa moja kutoka katika jami za wenyeji."

*"Baada ya kuishi na wakimbizi kama majirani zetu kwa takribani kipindi chote cha maisha yangu, ni jambo linalotia moyo kuona kwamba WFP imetoa fursa ili kuwasaidia wenyeji kupitia ununuaji na ugawaji wa chakula,"*

**Bw. Jackson Christopher, mkazi wa Wilaya ya Kakonko**

***Inaendelea Ukurasa wa 12***

*Kutoka ukurasa wa 11*

Huku kukiwa na uhakika kwamba WFP itanunua maharage yao, wakulima wanaosaidiwa na Enabel walihamasishwa kuzalisha maharage kwa kiwango na ubora wa kutosha. Mwaka huu, kupitia uratibu wa Enabel, jumla ya takribani tani za metriki 400 za maharage zilinunuliwa kutoka Vyama vya Ushirika vya Masoko ya Mazao ya Kilimo vya Nyakitonto na Muugano Kiziguzigu (AMCOS). Juhudi za kukusanya maharage ya vyama hivi zilifanyika katika wilaya nne za Kakonko, Kibondo, Kasulu na Uvinza za mkoani Kigoma.

Bw. Jackson Christopher, mkazi wa Wilaya ya Kakonko ni mwenyekiti wa sasa wa AMCOS ya Muungano. "Baada ya kuishi na wakimbizi kama majirani zetu kwa takribani kipindi chote cha maisha yangu, ni jambo linalotia moyo kuona kwamba WFP imetoa fursa ili kuwasaidia wenyeji kupitia ununuaji na ugawaji wa chakula," anasema Christopher. "Siku za nyuma, mwingiliano wetu kupitia soko na wakimbizi haukuwa rahisi, lakini ushirikiano huu na WFP umetuingiza katika hatua nyingine."

Maharage yaliyonunuliwa kwa zaidi ya Dola za Marekani 300,000 yatagawiwa katika miezi ijayo kwa wakimbizi wapatao 230,000 waliko mkoani Kigoma.

## UMASKINI NA MIIKO NI VIKWAZO KWA AFYA YA HEDHI YA WASICHANA ZANZIBAR



Mgogoro wa COVID-19, na hatua zinazofuatia za kujikinga vina uwezekano wa kukwamisha maendeleo ya juhudi za kutokomeza Ukeketaji (Tohara ya Wanawake) nchini Tanzania. ***Picha | Gonzalo Bell/UNFPA Tanzania***

Afaafa* (miaka 19) alipata hedhi yake ya kwanza takribani miaka sita iliyopita. Anakumbuka mama yake alivyomchukua kutoka nyumbani kwao huko Mwembe Njugu (karibu na Mji Mkongwe Zanzibar) hadi Makadara, ambako rafiki mpenzi wa mama yake, Maimuma, aliishi. Alikaa pale kwa sikut tisa akijifunza kuhusu umuhimu wa usafi binafsi wakati wa hedhi na ni jinsi gani ajisafishe damu za hedhi ikiwa ni pamoja na kutumia kitambaa, ambacho aliambiwa hakina budi kubaki cheupe kama ishara ya usafi. Pia aliambiwa "asicheze na wavulana" kwani angaliweza kupata ujauzito.

Ujumbe muhimu kabisa ambao Afaafa alisisitizwa kuukumbuka daima, hata hivyo, kiasi kwamba hata ikitokea akasahau vingine vyote ni kwamba suala la hedhi lilikuwa la aibu. Hakuna mtu anayepaswa kujua kabisa kwamba yeye yuko katika siku zake za hedhi, Bi Maimuna alimsisitiza: "hata mumeo hapaswi kufahamu hili." Aliambiwa pia kwamba vile vipande vya vitambaa alivyotumia kujisafisha vilipaswa kufichwa na kufuliwa na kukaushwa pasipo kuonwa na macho ya mtu mwingine yeyote.

*Inaendelea Ukurasa wa 13*

*Kutoka ukurasa wa 12*

Imepita miaka sita tangu mafunzo hayo ya unyago kutoka kwa Bi Maimuna, lakini kauli zake zikingali mbichi kwenye akili ya Afaafa. Yeye hugubikwa na hofu kila siku zake za hedhi zinapokaribia na miongoni mwa hofu zake kubwa ni kwamba huenda asimudu gharama za taulo za hedhi. Huwa anajaribu kutunza walau Shilingi za Tanzania 500 (kama centi 25 za Dola za Marekani) anazopewa kutumia awapo shuleni hadi ajikusanyie Shilingi 3,500 (kama Dola za Marekani 1.50) – kiasi kinachotosha kujinunulia taulo hizo, lakini mara nyingi sana hushindwa kufikia lengo lake na kujikuta akitumia vitambaa. Jambo hili humpa shinikizo zaidi maana shuleni kuna matundu mawili tu ya choo yanayotumiwa na zaidi ya wasichana 200. Kwa sababu hizi, Afaafa anasema anapokuwa hana taulo za hedhi, basi siku hizo za hedhi huamua kubaki nyumbani, “sitaki kujitia aibu mbele ya rafiki zangu”, anaongeza kusema.

Tanzania inapoendelea kukabiliana na janga la COVID-19, Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Idadi ya Watu (UNFPA) nchini Tanzania linaweka kipaombele mahitaji ya afya ya ngono na uzazi kwa wanawake na wasichana kama sehemu ya kusaidia juhudi za taifa katika mapambano dhidi ya janga hilo, ikiwemo kuhakikisha kwamba vituo 10 rafiki vya Mabalehe na Vijana vinavyosaidiwa na UNFPA kote Zanzibar vinakuwa wazi huku nafasi kati ya mtu na mtu ikizingatiwa na hatua za kuzuia maambukizi ya COVID-19 zikiheshimiwa. Vituo hivi ni muhimu sana kwa wasichana kama Afaafa, kwani vinawapa faragha wanayoihitaji, ambako wanaweza kufika na kupata taarifa sahihi na huduma kwa umri wao kuhusu masuala ya hedhi, wengi wao ikiwa ndiyo mara ya kwanza.

Changamoto ya COVID-19 hata hivi hatimaye itapita na katika kipindi cha kurejea kwenye ukawaida, UNFPA Tanzania itaendelea kuongeza juhudi ili kuhakikisha kwamba hakuna msichana anayezuiwa katika safari yake ya kutaka kutimiza ndoto yake, matamanio na kukuza vipawa vyake kikamilifu ifikapo mwaka 2030.

## WHO TANZANIA YATOA MSAADA WA KIUFUNDI KWA ZANZIBAR KWA UGATUZI WA JUHUDI ZA KUKABILIANA NA COVID-19

Mwezi Machi, 2020 ndiyo kipindi ambapo maambukizi ya COVID-19 yaligunduliwa nchini na serikali kuamua kufunga taasisi zote za elimu, kusitisha shughuli za michezo, mikutano ya kisiasa na ndege za kimataifa. Hata hivyo, tangu Mei, 2020, nchi imeonyesha kupungua kwa maambukizi, hivyo katikati mwa mwezi Juni, hatua hizo za usitishaji zilianza kufunguliwa hatua kwa hatua.

Kutokana na taarifa zilizopo, huenda COVID-19 itaendelea kubaki miongoni mwetu kwa muda mrefu zaidi. Kwa hiyo, mifumo ya afya nchini Tanzania inazidi kukabiliana na ukweli huu na kuingiza huduma za COVID-19 katika utaratibu wake katika ngazi za vituo vya afya vya wilaya na kuendelea na huduma nyingine muhimu, hivyo kuhamisha hatua za usimamizi kutoka katika serikali kuu kwenda katika ngazi za chini.

Kufuatia hatua hizi za sera ya ugatuzi, Wizara ya Afya ya Zanzibar imeteua vituo vya afya kwa ajili ya kushughulika na COVID-19 katika kila wilaya. Vituo hivi vitawatenga washukiwa wa maambukizi, kuchukua sampuli zao ili zifanyiwe vipimo na kuwahudumia kwa namna inayostahili. Wale wagonjwa watakaozidiwa watahamishiwa katika vituo vya matibabu vya ngazi ya rufaa.

*Inaendelea Ukurasa wa 14*

*Kutoka ukurasa wa 13*

Wizara ya Afya kwa msaada wa kiufundi kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) imeandaa mwongozo wa kiufundi katika maeneo yote matano ya uchukuaji hatua, yaani: uratibu, ufuatiliaji, huduma kwa mgonjwa na kinga na udhibiti wa maambukizo, utoaji taarifa ya hatari na ushirikishjaji wa jamii na taratibu za lojistiki (itifaki).

"Tunatamani kwamba kila kituo cha afya cha Zanzibar kiwe na uwezo wa kubaini, kukusanya sampuli na kutoa huduma kwa ugonjwa wa COVID-19. Huenda maambukizi yakapungua sasa lakini yakaja kuongezeka baadaye. Kwa hio, tunahitaji kuzijengea uwezo timu zetu za usimamizi za wilaya, vituo vyetu vya afya na wanaojitolea katika masuala ya afya ili kubaini washukiwa wa ugonjwa, kuwatenga na hata kuchukua sampuli," alisema Meneja wa Kituo cha Utoaji Huduma za Dharura, Dkt. Hussein Haji.

Kwa mujibu wa Dkt. Haji, vituo vilivyoteuliwa kwa ajili ya COVID-19 katika wilaya vimebainishwa huko Unguja na Pemba, ambapo kwa upande wa Unguja timu za watoa huduma za afya zimepatiwa mafunzo katika kubaini maambukizo, kutoa huduma kwa wagonjwa na taratibu za IPC. Katika awamu ya pili, mafunzo yatatolewa kwa watumishi wa afya walioko Pemba.

Njia hii mpya inatarajiwa kuwa na ufanisi zaidi kwani huduma zilizopo katika mifumo ya afya itatumika kuimarisha matunzo kwa wagonjwa wote. Kwa kuongezea, watumishi wa kujitolea wa afya ya jamii wapatao 500 ambao walipatiwa mafunzo hapo awali ili kwenda katika ngazi ya kaya kusaidia katika utoaji huduma kwa mama na mtoto wamepewa mafunzo mapya ili kusaidia katika kutoa huduma ya kufuatilia wote wanaoshukiwa kwa COVID-19.

"Shirika la WHO liko tayari kutoa msaada wa kiufundi na kifedha ili kuimarisha mwitikio dhidi ya COVID-19. Vilevile tunashirikishana ushahidi na maarifa mapya kadiri hali inavyobadilika. Ni muhimu sana kuhakikisha kwamba mifumo yetu ya afya kwa ujumla wake iko tayari kukabiliana na dharura za kiafya," alisema Dkt. Tigest Ketsela Mengestu, Mwakilishi wa WHO nchini.




Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani nchini Tanzania, Dkt. Tigest Ketsela Mengestu, akikabidhi msaada wa dawa kwa Dkt. Elias Kwesi, Mkurugenzi wa Kitengo cha Utayari wa Dharura cha Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto jijini Dar es Salaam. ***Picha | WHO Tanzania***

*Inaendelea Ukurasa wa 15*

*Kutoka ukurasa wa 14*




Wakati janga la COVID-19 lilipokuwa likitikisa sana, wanajamii walizingatia tabia za kijikinga, zikiwemo kunawa mikono kutumia maji yanayotiririka kutumia vifaa vilivyowekwa katika maeneo ya biashara na ya umma, kama hiki kilichokutwa katika Kituo cha Mabasi ya Mjini cha Makunduchi huko Zanzibar. ***Picha | WHO Tanzania***




Vibarua na wafanyakazi wa WHO wakipakua makasha yenye misaada ya dawa na vifaa tiba vilivyonunuliwa na kutolewa kwa Serikali jijini Dar es Salaam. ***Picha || WHO Tanzania***

# KUADHIMISHA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA (DAC) KUPITIA WEBINAR MAALUMU YA WAJENGA USHAWISHI

## DAY OF THE AFRICAN CHILD WEBINAR WITH UNICEF TANZANIA PARTNERS




Bango rasmi kwa ajili ya kongamano la mtandaoni la Siku ya Mtoto wa Afrika lililoandiwa ili kuelewa wajibu ambao UNICEF na washirika wetu wengi wanaoutimiza ili kuwasaidia watoto na vijana, hasa baada ya 'mabadiliko makubwa ya kijamii' katika kipindi cha baada ya COVID-19. ***Picha | UNICEF Tanzania***

Tarehe 16 Juni ya kila mwaka hutoa fursa ya kuwakumbuka maelfu ya vijana, watoto mashujaa waliofanya maandamano huko Soweto, Afrika ya Kusini, mwaka 1976 ili kupinga ubaguzi wa rangi na kudai usawa katika elimu. Fundisho walilotuachia watoto hawa mashujaa, ambapo wengi wao walipoteza maisha, linaendelea kujenga kesho iliyo bora kwa watoto kote barani Afrika leo. Siku ya Mtoto wa Afrika inabeba maana kubwa zaidi mwaka huu wakati dunia inapokabiliwa na changamoto kubwa ya virusi vipya. Mwaka huu, ili kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, UNICEF Tanzania iliandaa kongamano maalumu kupitia jukwaa la mtandaoni (webinar) kwa kuhusisha wajenga ushawishi wetu walio wengi ili kuelewa jukumu kuu ambalo UNICEF na washirika wetu wengi wanatekeleza ili kuwasaidia watoto na vijana, hasa katika kipindi cha baada ya COVID wakati ambapo shule na vyuo vikuu vinafunguliwa na watoto wanarejea kwenye mazingira yaliyojawa na 'tararibu mpya za uendeshaji maisha'.

Katika kongamano hilo la mtandaoni, wadau mbalimbali kutoka tasnia ya teknolojia, habari na sekta binafsi walishiriki ambapo tukio zima liliongozwa na Mariam Mmbaga, ambaye anajitolea katika Umoja wa Mataifa kupitia UNICEF.

Bw. Raphael Denis, ambaye ni msimulizi wa digitali wa UNICEF na mwamba kijana anayetetea haki za watoto na vijana nchini Tanzania alifungulia majadiliano kwa kuangazia namna vijana wanavyotekeleza wajibu wa uongozi katika kipindi hiki cha janga la virusi nchini Tanzania.

*Inaendelea Ukurasa wa 17*


*Kutoka ukurasa wa 16*

Aliangazia namna vijana wanavyotekeleza majukumu muhimu kwa kutumia fursa ya zana za habari za kidijitali katika kushirikishana taarifa na kukuza uelewa wa watu. Bw. Given Edward, mjasiriamali wa kijamii na bingwa katika masuala ya kidijitali alizungumzia kuhusu namna waelimishaji wanavyoweza kuandaliwa na kutumia teknolojia ili kuimarisha ujifunzaji. Alisisitiza kwamba, janga lililopo sasa limefanya kuwe na ulazima wa kushughulikia mgawanyiko wa kidijitali uliopo nchini ili kwamba vijana wengi zaidi Watanzania wapate fursa sawa za kujifunza na kuingia katika masuala ya ubunifu.

Bw. Neville Meena, Katibu Mkuu, Jukwaa la Wahariri Tanzania aliangazia wajibu wa vyombo vya habari katika kuendeleza haki za watoto kwa kuendelea kukazia habari za maendeleo. Bw. Hassan Ali Mzee, Mwenyekiti wa Chama cha Waongoza Watalii cha Zanzibar (ZATO) alizungumzia wajibu wa sekta binafsi na hata ya upande wa utalii katika kutimiza majukumu yanayoheshimu na kuimarisha haki za watoto.

Bi. Pamela Shao, ambaye ni mkuu wa UNICEF mkoani Mbeya, anayesimamia na kuongoza ahadi za kiprogramu za UNICEF katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe, alitoa picha ya jumla kuhusu Siku ya Mtoto wa Afrika ina maana gani kwa UNICEF nchini Tanzania na ni kwa namna gani kihistoria UNICEF imewawezesha watoto na vijana kusimimia haki zao. Vilevile, alizungumzia msaada wa UNICEF kwa Serikali katika kutoa mwitikio kwa janga na jinsi shirika linavyowawezesha watoto na vijana kuwa washirika wenye ufanisi katika kuendeleza ajenda ya hazi wa watoto nchini.


Wanajukwaa wote hawa walijibu maswali kutoka kwa hadhira kabla kipindi hicho kilichodumu kwa saa nzima kufika mwisho. Kongamano hilo la mtandaoni lilitangazwa mubashara kupitia mitandao ya kijamii ambapo lilifuatiliwa na watu wapatao 5,000 ambao waliingia kupitia Facebook ili kufuatilia. Tazama rekodi yake hapa ikiwa hukupata fursa ya kufuatilia mbashara.



Tuliwakaribisha washawishi wa jamii sita kwenye kongamano la mtandaoni ambalo liliadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika. ***Picha | UNICEF Tanzania***

*Inaendelea Ukurasa wa 18*

Kutoka ukurasa wa 17



Msimulizi wa hadithi kupitia njia ya kidijitali wa kutoka UNICEF, Raphael Denis, aliyezungumzia kuhusu nguvu ya vijana kama mawakala wa mabadiliko ili kuikuza zaidi Afrika. Hii ilikuwa katika kongamano la mtandaoni lililoandaliwa na UNICEF Tanzania. ***Picha | UNICEF Tanzania***

## SERIKALI NA IOM ZAENDESHA TATHMINI YA UTAYARI WA VITUO VYA MIPAKANI KUHUSU AFYA

Shirika la Kimtaifa la Wahamiaji (IOM) ambalo liko chini ya Umoja wa Mataifa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Wizara ya Afya, Zanzibar ziliandaa tathamini ya utayari na mahitaji kwa kukazia vituo muhimu vya mpakani (POEs) pamoja na vituo vya afya vilivyo jirani katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Mbeya, Mwanza na Songwe upande wa Tanzania Bara na Unguja na Pemba, upande wa Zanzibar.

Kwa msaada wa kifedha kutoka Serikali ya Japan na Shirika la Misaada ya Kimaendeleo la Uingereza (DFID), tathmini hiyo ilibaini mahitaji ya kiuwezo na upungufu uliopo katika POE kwa maana ya watumishi na vifaa ili kuwakagua na kuwapima wasafiri kwa ajili ya huduma za rufaa pale inapohitajika. Hii ilihusisha vituo rasmi vya mpakani na vile visivyo rasmi ambayo wageni hutumia kuingia nchini. Tathmini hii ilionyesha kwamba ni vituo vichache vya mpakani ndiyo vilikuwa na seti kamili ya kitabibu kwa ajili ya kujikinga dhidi ya maambukizo (PPE), kuwa na maeneo ya kutosha ya kunawia mikono, vyumba maalumu vya kutenga wahisiwa wa ugonjwa au majengo ya kudumu kwa ajili ya ufuatiliaji wa masuala ya afya, vituo vya kutakatisha na vyombo maalumu vya kutupia uchafu hatari wa kibiolojia Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa kutumia mapendekezo yaliyotokana na tathmini hiyo katika Vituo vya Mpakani, IOM imeanza kufanya manunuzi na kutoa vifaa kwa ajili ya kunawia mikono sambamba na kutoa vifaa vya kupimia.

Mwezi Juni, 2020, IOM ilitoa vifaa vya kunawia mikono kwenye Vituo 20 vya Mpakani na vituo vya afya 11 katika Mkoa wa Kigoma lakini pia ilitoa vifaa vya kunawia mikono

Inaendelea Ukurasa wa 19

*Kutoka ukurasa wa 18*

katika vituo 28 vya mpakani na vituo 5 vya afya huko katika Visiwa vya Unguja na Pemba.



Tathmini ya Kituo cha Mpakani (PoE) kisicho rasmi ikiendelea katika Soko la Samaki la Ngalawa Bububu Kihinani, Unguja. ***Picha | IOM Tanzania/Nuwe Blick***

“Asanteni sana kwa kutuletea vifaa hivi vya kunawia mikono vikiwemo ndoo, vitakatishi mikono na sabuni, tutaviweka katika maeneo ya kuingilia na kutokea katika POE kwa ajili ya watumishi wetu na wageni/wahamiaji ili wapate kunawa mikono kabla ya kuingia na kutoka katika POE. Jambo hili siyo tu kwamba litaimarisha hatua zetu za kinga dhidi ya COVID-19 lakini pia kuzuia magonjwa mengine ya kuambukiza,” alisema Masunga Simoni, ofisa anayesimamia Kituo cha Mpakani cha Manyovu katika Mkoa wa Kigoma.

“Tunawashukuru sana IOM kwa msaada wa vifaa vya kunawia mikono katika POE yetu. Kituo chetu cha Mpakani kina vitengo viwili kile cha mnada wa samaki na kingine kwa ajili ya wasafiri waendao na kutoka Mombasa, Kenya hadi Micheweni, kwa hiyo vifaa hivi vitasaidia sana wasafiri na sisi wenyewe kijikinga dhidi ya magonjwa kama vile COVID-19, na Kipindupindu.’’ Alisema Dkt. Suleiman Faki, Ofisa wa Afya ya Mazingira katika Kituo cha Mpakani kisicho rasmi cha Micheweni, Pemba.




Timu ya tathmini katika Kituo cha Afya cha Kizimkazi Dimbani. ***Picha | IOM Tanzania/Nuwe Blick***



Hema kwa ajili ya wahisiwa wa ugonjwa wa COVID-19 katika kituo cha mpakani (PoE) kilichopo katika Kiwanja cha Ndege cha Pemba. ***Picha | IOM Tanzania/Nuwe Blick***

## SIKU ZIJAZO ZA KIMATAIFA:

**Julai 18-** Siku ya Kimataifa ya Nelson Mandela

**Julai 28 –** Siku ya Kimataifa ya Homa ya Ini

**Julai 30 –** Siku ya Kimataifa ya Kifua Kikuu

**Agosti 12 –** Siku ya Kimataifa ya Kupambana dhidi ya Ulanguzi

**Agosti 19 –** Siku ya Kimataifa ya Kibinadamu Duniani

## UMOJA WA MATAIFA MADHUBUTI KWA DUNIA BORA ZAIDI

UNITED NATIONS
TANZANIA

**Ofisi ya Mratibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa**

+255 22 219 5021

info.untz@one.un.org

Website: tanzania.un.org

This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021